TANGAZO LA SERIKALI NA. 838 la tarehe 11/10/2024

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA
(SURA. 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 128 (2))*

## AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA NDEGE MBILI ZISIZO NA RUBANI ZINAZOINGIZWA NCHINI NA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Ndege Mbili Zisizo na Rubani zinazoingizwa nchini na Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika kuanzia tarehe 27 Agosti, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana Ndege mbili zisizo na rubani zilizoainishwa katika Jedwali, zinazoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na Wizara ya Maliasili na Utalii unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo Ndege (Drones) husika zitatatumika kwa matumizi tofauti au zitahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itakoma kutumika tarehe 26 Februari, 2025

JEDWALI

*(Imetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Idadi | Mahali Ziliponunuliwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Israel Drone DR750 with Thermal Imaging Camera for Day and Night Conditioning with Training up to 15 Km and 1H Flight Time. | 2 | Zinaingizwa Nchini |

Dodoma,
3 Oktoba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*